



**OFISI YA RAIS TAMISEMI  
HALMASHAURI YA MJI KONDOA  
TOLEO MAALUM LA MBIO ZA  
MWENGE WA UHURU 2019**



## Mwenge wa Uhuru wakimbizwa Kondo Mji



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondo Msoleni Dakawa (Mwenye miwani) akipokea Mwenge wa Uhuru kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondo Mustapha Semwaiko tayari kwa kukimbizwa katika Halmashauri ya Mji Kondo

### SERA YA UHARIRI

Madhumini ya Jarida hili ni kuhabarisha na kuelimisha wananchi juu ya shughuli mbalimbali zinazofanywa na Halmashauri ya Mji Kondo. Aidha Sera, Mipango na utekelezaji wa miradi ya maendeleo inafafanuliwa kupitia jarida hili. Isipokuwa pale inapokatazwa habari za Jarida la Halmashauri ya Mji Kondo zinaweza kunukuliwa mradi Mhariri ajulishwe kwa maandishi.

## SHUKRANI KUTOKA KWA MKURUGENZI

**Bodi ya Uhariri**

Msoleni Dakawa

Sekela Mwasubila

Kaunga Amani

Adrian Kikoti

**Mawasiliano**

S.L.P 711 Kondoaa

Simu: +255 712264912

Nukushi: +255262360313

**Mitandao ya Kijamii**Barua Pepe:  
td@kondoatc.go.tzTovuti  
www: kondoatc.go.tzFacebook  
Kondoaa TCInstagram  
kondoatc2015**Msoleni Dakawa****Mkurugenzi Halmashauri ya Mji**

Natoa shukrani za dhati kwa Mhe. Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli kwa kutuma vijana mahiri na wazalendo kuweza kumuwakilisha kikamilifu kukimbiza Mwenge wa Uhuru nchi nzima na kuhakikisha wanafikisha ujumbe wa Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2019 kwa wananchi unaosema:- *“Maji ni haki ya kila Mtu, tutunze vyanzo vyake na tukumbuke kushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa”*

Pia natoa shukrani kwa viongozi wa Wilaya wakiongozwa na Jemedari Mahiri Mkuu wa Wilaya ya Kondoaa Mheshimiwa Sezaria Veneranda Makota, Waheshimiwa Madiwani, Mbunge Mheshimiwa Edwin Sannda, Wakuu wa idara na watumishi wote kwa ujumla. Umuhimu wa kipekee kabisa kwa wananchi wa Halmashauri ya Kondoaa Mji kwa ushirikiano mkubwa na mapokezi mazuri ya Mbio za Mwenge wa Uhuru 2019.

Mwenge wa Uhuru wa mwaka 2019 umekimbizwa jumla ya kilomita 67.5 ambapo umepitia Miradi 6 yenye thamani ya shilingi 998,079,014.74 miradi hiyo ni ya Sekta ya Afya shilingi 418,980,000.00 Maji shilingi 142,565,854.74 Elimu shilingi 270,295,160.00, Ujenzi shilingi 165,238,000.00, Maliasili shilingi 1,000,000.00. Katika fedha hizo Shilingi milioni 591,238,000.00 ni fedha kutoka Serikali Kuu, shilingi 912,013.74 ni fedha toka Halmashauri, shilingi 30,755,000.00 nguvu za wananchi, na shilingi 375,174,001.00 ni mchango wa wahisani mbalimbali wa maendeleo.

Mwisho, niwashukuru sana wakimbiza Mwenge Kitaifa wakiongozwa na Ndugu Mzee Mkongea Ali na wakimbiza Mwenge kimkoa niseme maoni na ushauri wenu tumepokea na tunaenda kufanyia kazi. Niwakaribishe tena katika Halmashauri ya Mji Kondoaa.

## ELIMU YA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA



Mkimbiza Mwenge kitaifa Mzee Mkongea Ali akishauri jambo kwa Afisa Uchaguzi Halmashauri ya Mji Kondo Robert Mashala katika viwanja vya Kolo Mnadani ulipopokelewa Mwenge wa Uhuru 2019 ikiwa ni sehemu ya uhamasishaji wa uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajia kufanyika mwezi Oktoba 2019.

### SIFA ZA MGOMBEA

1. Awe raia wa Tanzania,
2. Awe na umri wa kuanzia miaka 21 na kuendelea,
3. Awe na uwezo wa kusoma na kuandika Kiswahili au Kiingereza,
4. Awe na kipato halali cha kumwezesha kuishi,
5. Awe ni mwanachama na amedhaminiwa na chama cha siasa,
6. Awe hajapatikana na hatia kwa kosa la utovu wa uaminifu na kuhukumiwa adhabu ya kifungo cha miezi sita au zaidi au adhabu ya kifo,
7. Hana ugonjwa wa akili uliothibitishwa na Daktari anayetambulika na serikali au Bodi ya Utabibu.

### SIFA ZA MPIGAKURA

1. Awe raia wa Tanzania,
2. Awe na umri wa miaka 18 na kuendelea,
3. Awe mkazi katika Mtaa husika,
4. Awe amejiandikisha kupiga kura,
5. Hana ugonjwa wa akili uliothibitishwa na Daktari anayetambulika na serikali au

### NAFASI ZINAZOGOMBEWA

**Mwenyekiti wa Mtaa.** Nafasi moja (1) kwa kila Mtaa

**Ujumbe wa serikali ya Mtaa.** Kila Mtaa nafasi sita (6) kati ya hizo nafasi mbili (2) ni za wanawake (Viti maalum).

## UJUMBE WA MWENGE KATIKA UZINDUZI WA MADARASA SHULE YA SEKONDARI YA KOLO

### Na. Sekela Mwasubila – Afisa Habari

Mwenge wa Uhuru umezindua madarasa mawili yenye madawati uliopo katika Shule ya Sekondari ya Kolo mradi uliogharimu kiasi cha shilingi milioni 36 ambapo serikali ilitoa shilingi milioni 25 na wananchi wali changia shilingi milioni 11.

Akitoa ujumbe wa Mwenge baadaya ya uzinduzi wa mradi mmoja wa wakimbiza Mwenge kitaifa Ndugu Kenani Kihongosi aliwapongeza wasimamizi wa mradi kwa kukamilisha mradi vizuri na kutumia fedha vizuri hadi mradi umekamilika.

Aliongeza kwa kuwasihi watumiaji wa mradi huo kuutunza ili utumike kwa muda mrefu na kutimiza lengo la serikali la kujenga madarasa hayo ambapo kwa sasa tatizo la uhaba wa madarasa litasahaulika.

Aliendelea kuwasihi wananchi na viongozi kuendelea kuunga mkono juhudi za serikali ya awamu ya tano kwa kufanya kazi kwa bidii na kulipa kodi ili serikali iendeleo kupata mapato na kuendeleza miradi mikubwa ina-yotekelezwa na serikali.

Serikali inatekeleza miradi mikubwa kwasasa ikiwemo mradi wa ufuaji umeme katika mto Rufiji, ujenzi wa reli ya kisasa, ujenzi wa mada-raja makubwa, utengengenezaji wa meli, unuzi wa ndege na ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami hivyo tumuunge mkono Rais wetu kwa kulipa kodi ili yote hayo yafanikiwe zaidi.

Hata hivyo alieleza kuwa mwenge wa uhuru umekuja na kaulimbiu mbalimbali za kupiga vita maambukizi mapya ya ugonjwa wa UKIMWI, Malaria, Rushwa na Madawa ya Kulevya.



Wakimbiza Mwenge kitaifa wakikagua wakikagua nyaraka za ujenzi wa madarasa mawili katika Shule ya Sekondari Kolo na kuhoji maswali kwa Mhandisi wa Ujenzi Kedmon Malima (aliyeinama).



Mkimbiza Mwenge kitaifa Ndugu Kenani Kihongosi akizungumza na wananchi wa Kolo na viongozi mbalimbali waliojitokeza kwenye uzinduzi wa mradi wa madarasa Kolo Sekondari.



Mkuu wa Wilaya ya Kondoa Mhe. Sezaria Makota akitoa shukrani kwa kiongozi wa mbio za Mwenge baada ya kuzindua mradi wa madarasa Kolo Sekondari.

## MRADI WA MAJI NA UKARABATI WA MIUNDOMBINU KATIKA ZAHANATI YA KOLO YAWARIDHISHA WAKIMBIZA MWENGE



Mkimbiza Mwenge Kitaifa Mzee Mkongea Ali akiangalia jiwe la ufunguzi wa Mradi wa Ukarabati wa Miundombinu na maji katika Zahanati ya Kolo baada ya kuzindua mradi huo.



Meneja wa Maji Wilaya ya Kondoakitoa maelezo ya mradi kwa wakimbiza mwenge kitaifa



Mwenge wa Uhuru ulipowasili katika Zahanati ya Kolo



Wakimbiza Mwenge kitaifa wakikagua nyaraka za mradi

## MBIO ZA MWENGE ZAPONGEZA VIJANA KUTUNZA MAZINGIRA



Mkimbiza Mwenge Kitaifa Ndugu Mzee Mkongea Ali (Wa kwanza kushoto), Mkuu wa Wilaya ya Kondoza Mhe. Sezaria Makota na Mkurugenzi wa Mji Msoleni Dakawa (nyuma) wakielekea eneo la mradi ambapo mizinga ya nyuki itawekwa.



Mkimbiza Mwenge Kitaifa Mzee Mkongea Ali waki-zindua mradi wa ufugaji nyuki katika Msitu wa Chemchem Kondoza Mjini wakati wa mbio za mwenge katika Halmashauri ya Mji Kondoza.



Mkimbiza Mwenge kitaifa Mzee Mkongea Ali (wa kwanza kulia) akitundika mzinga katika msitu wa Chemchem Kondoza.

**Na: Sekela Mwasubila - Afisa Habari**

Kiongozi wa mbio za Mwenge 2019 Mzee Mkongea Ali amewapongeza kikundi cha vijana walioamua kufanya kazi ya kulina asali katika msitu wa Chemchem uliopo Kondoza Mjini kwani kwa kufanya hivyo watatunza mazingira ya msitu huo na kuwa endelevu kwa kipindi kirefu.

Pongezi hizo alizitoa wakati wa uzinduzi wa mradi huo kwa vijana 10 ambao walikabidhiwa mizinga kumi ya nyuki baada ya kupata fedha kutoka Halmashauri ya Mji ikiwa ni sehemu ya asilimia kumi ya mapato ya ndani.

Aidha aliwasihi wananchi kuendelea kuhakikisha wanaendelea kutunza vyanzo vya maji kwa kupanda miti kwa wingi ili kuondokana na tatizo la kukosekana kwa maji safi na salama katika maeneo yao.

“Wazee wetu walitunza vyanzo vyetu toka zamani na ndio maana tunaendeleo kufaidika hadi leo hata uje ukame wa namna gani hivyo tuendeleo kuvitunza vyanzo vyetu na kupanda miti katika vyanzo vingine ili kuwa na maji ya uhakika.” Alisisitiza Ndugu Mkongea Ali.

Akiongea kwenye mbio hizo Mkuu wa Wilaya ya Kondoza Mhe. Sezaria Makota aliwahakikishia wakimbiza Mwenge kuwa wataendelea kutunza vyanzo vya maji na kuhamasisha upandaji wa miti katika vyanzo vya maji ili kutunza vyanzo hivyo.

Mwenge wa Uhuru ulizindua mradi huo ambao umegharimu kiasi cha shilingi milioni moja ambao ni mkopo kutoka Halmashauri ya Mji na vijana hao watarudisha fedha hizo ndani ya mwaka mmoja.

## Historia ya Chemchem ya Maji Kondoza Mjini ya- wavutia wakimbiza Mwenge



Wakimbiza Mwenge kitaifa wakisikiliza maelezo ya Chemchem ya Kondoza Mjini kutoka kwa mlinzi wa eneo hilo wakati wa uzinduzi wa mradi wa ufugaji nyuki kwa Vijana wakati wa mbio za Mwenge wa Uhuru katika Mji wa Kondoza.



Mmoja wa wakimbiza Mwenge Ndugu Malugu Mwanganya akiwa mbele ya Chemchem ya Maji Kondoza Mjini ikiwa pia ndio chanzo cha maji kinachotegemewa na wakazi wa Kondoza Mjini.

## Mradi wa Madarasa na Vyoo St. Gemma wazinduliwa



Moja ya jengo la madarasa lililopo katika Shule ya Mtakatifu Gemma Kondoa ambalo lilizinduliwa na mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2019.



Msoma taarifa ya mradi akimkabidhi mkimbiza mwenge Kitaifa taarifa ya mradi baada ya kuisoma.



Mkimbiza Mwenge Kitaifa Ndugu Mzee Mkongea Ali akiangalia jiwe la msingi baada ya kuzindua mradi wa madarasa katika Shule ya Mtakatifu Gemma. Picha ya Chini akiongea na hadhara .

**MRADI HUU ULIKUWA NI WA UZ-  
INDUZI WA MADARASA 5 NA VYOO  
9 MRADI ULIOTEKELEZWA KWA  
GHARAMA YA SHILINGI MILIONI  
233.5**





## Mwenge wa Uhuru waweka Jiwe la Msingi Kituo cha Afya Kingale



Mkimbiza Mwenge Kitaifa Mzee Mkongea Ali akiweka jiwe la Msingi katika ujenzi wa Kituo cha Afya Kingale.

Mkimbiza Mwenge Kitaifa Ndugu. Malugu Mwanganya (wa kwanza Kushoto) akitoa ushauri kwa Mhandisi wa Ujenzi wa Hlmashauri ya Mji (Mwenye nguo ya bluu) katika jingo la mochwari kituo cha Afya Kingale.



Kushoto ni jengo la upasuaji katika Kituo cha Afya Kingale ikiwa ni moja ya majengo matano katika kituo hicho.

Chini ni jengo la mama na mtoto katika kituo cha Afya Kingale



Mwenge wa Uhuru uliweka Jiwe la Msingi katika Kituo hicho na mradi huu umegharimu kiasi cha shilingi milioni 418,000,000 ambapo serikali ilitoa shilingi milioni 400 na wananchi shilingi milioni 18.

Mradi huu una majengo matano ambayo ni jengo la maabara, jengo la upasuaji, jengo la mama na mtoto, Mochwari na nyumba ya daktari.



## MATUKIO KATIKA PICHA ENEO LA MAPOKEZI KOLO MNADANI



Mkuu wa Wilaya Mhe. Sezaria Makota akiwasili eneo la mapokezi



Mkurugenzi wa Mji Msoleni Dakawa (alieruka juu) akicheza pamoja na watumishi eneo la mapokezi



Waheshimiwa Madiwani, Afisa Tarafa na Watumishi wa Halmashauri ya Mji Kondoak wakishangilia kwa pamoja ujio wa Mwenge wa Uhuru eneo la Mapokezi



Mkimbiza Mwenge Kitaifa Ndugu Latifa Juwakali akipokelewa na Mkuu wa Wilaya Mhe. Sezaria Makota kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kondoak



Mkuu wa Wilaya ya Kondoak Mhe. Sezaria Makota akiwa amebeba Mwenge wa Uhuru mara baada ya kuwasili katika Halmashauri ya Mji Kondoak



Mkimbiza Mwenge Kitaifa Ndugu Haji Hamad akisalimiana na Afisa Uhamiaji mara baada ya kukaribishwa katika Halmashauri ya Mji Kondoak.

## MATUKIO KATIKA PICHA ENEO LA MKESHA KITUO CHA AFYA KINGALE



Mkimbiza Mwenge Kitaifa Ndugu Mzee Mkongea Ali akimsikiliza mtaalam wa Afya akitoa elimu ya uzazi wa mpango eneo la mkesha wa mwenge Kituo cha Afya Kingale



Mkimbiza Mwenge Kitaifa Ndugu Mzee Mkongea Ali akimsikiliza mtaalam wa Afya akitoa elimu ya ugonjwa wa Malaria eneo la mkesha wa mwenge Kituo cha Afya Kingale



Mkimbiza Mwenge Kitaifa Ndugu Mzee Mkongea Ali akimsikiliza mtaalam wa Ardhi akitoa elimu upimaji ardhi eneo la mkesha wa mwenge Kituo cha Afya Kingale



Mkimbiza Mwenge Kitaifa Ndugu Nkwimba Nyangogo akiawaaga viongozi na watumishi wa Halmashauri ya Mji Kondo baada ya kumaliza kukimbiza mwenge katika halmashauri ya Mji Kondo na kuelekea Wilaya ya Bahi



Mkuu wa Wilaya ya Kondo Mhe. Sezaria Makota akimkabidhi Mwenge wa Uhuru Mkuu wa Wilaya ya Bahi Mhe. Mwanahamisi .. Baada ya kumaliza mbio zake Wilaya ya Kondo



Baadhi ya wakimbiza Mwenge Kitaifa wakiwa katika picha ya pamoja eneo la makabidhiano ya mwenge Kijiji cha Zamahero baada ya kumaliza mbio zake halmashauri ya Mji Kondo.